
SIKU
ZA UJANA WANGU
James Kalekwa

# SIKU

# ZA

# UJANA

# WAKO.

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Siku za Ujana: Utangulizi....................................................... 3

Awamu tatu za maisha:.........................................................4

a) Awamu ya utoto........................................................ 5

b) Awamu ya ujana......................................................... 7

c) Awamu ya uzee......................................................... 9

Viwekezo ndani ya siku za Ujana:........................................ 10

Kuna mambo ni ya Ujana tu:...............................................15

**Hitimisho**......................................................................... 18

**Kuhusu Mwandishi**............................................................ 19

**Kuhusu New Vine Church**...................................................19

**Mawasiliano na Mwandishi**...............................................20

# Siku za Ujana: Utangulizi

*"Mkumbuke muumba wako* ***siku za ujana wako****, Kabla hazijaja siku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka uakaposema mimi sina furaha katika hiyo."* Mhubiri 12:1

Biblia inaonyesha ya kwamba kuna kipindi kwenye maisha haya ambacho kimepewa jina la "siku za ujana wako". Maana yake kuna siku zingine pia. Walau kutokea kwenye andiko hili tunaona kuna siku zilizo mbaya. Hazijaitwa jina ni siku za nini hasa.

Kwenye siku za ujana kuna jambo linapaswa kutokea kwenye maisha ya kijana husika. Jambo hilo ni kumkumbuka muumba!

Kwanini umkumbuke muumba wako siku za ujana wako? Kwanini isiwe siku zingine? Na kwa nini siku za ujana ndiyo muafaka? Kuna nini hasa kwenye siku hizi? Muumba wako ana nini cha kufanya na siku hizi?

Ni safari fupi na tamu ya kuyajibu maswali haya… karibu!

# Awamu tatu za maisha:

Ni vyema ukatambua ya kwamba majira na nyakati ni jambo halisi kwenye maisha ya mwanadamu na ulimwengu. Kuna majira na nyakati ambayo ni binafsi kwa mtu. Lakini, kwenye kitabu hiki ninataka kukujengea uelewa juu ya majira na nyakati yaliyowekwa tayari kwenye maisha ya mwanadamu ambamo yeye atatiririka kuyaelekea.

Swala la nyakati kwenye kitabu hiki, litajielekeza kuangalia kigezo cha makuzi. Na kitakuwa kimegawanywa kwenye sehemu kubwa tatu: *utoto, ujana na uzee.*

Sasa, kibiblia, majira na nyakati si tu huja na kuondoka. Bali kila majira na wakati vimebeba ajenda ambazo zinapaswa kutokea humo.

*"Kwa kila **jambo** kuna majira yake, na wakati kwa kila **kusudi** chini ya mbingu."* Mhubiri 12:1

Ukisikia kuna majira, basi uwe na uhakika kuna jambo linapaswa kutokea humo; na ukiona wakati basi tambua ya kwamba kuna kusudi linapaswa kutendeka hapo.

Kwa msingi huo basi, nitakapokuwa nikikueleza “majira na nyakati” za wanadamu vilevile nitakuwa ninakueleza “mambo na makusudi” yanayopaswa kutokea humo.

Uko tayari kuutambua ugunduzi huu wa nyakati? Basi tuambatane pamoja kwenye safari hii nzuri na ya thamani.

### a) Awamu ya utoto

*“Wana wa wana ndio taji ya wazee,* ***Na utukufu wa watoto ni baba zao.”*** Mithali 17:6

Hiki ni kipindi ambacho kwa umri tunaweza kukigawanya baina ya miaka ya awali kabisa mwanadamu anapozaliwa mpaka umri wa miaka kumi na nne. Hawa wanaweza kuingia kundi moja. Hata hivyo, humo ndani ya kundi kuna mgawanyo mwingine mwingi. Si lengo langu hasa kujielekeza kujadili humo ndani.

Awamu hii ya maisha, ni kipindi ambacho mtoto hana maisha yake mwenyewe ya kujitegemea. Chochote alichonacho huja kuhusianishwa na wazazi wake – na baba yake, “…na utukufu wa watoto ni baba zao.”. Utukufu maana yake ni kufunuliwa, kuwekwa wazi, kujulikana, kuonekana au kudhihirika. Hiki ni kipindi ambacho mtoto huishi kwa jina la baba yake tu. Ni kipindi cha utegemezi wa mahitaji mbalimbali. Mtoto huhitaji kwa utegemezi maswala ya kimwili, kinafsi na

kiroho; huyatazamia kuamuliwa na kuelekezwa kutoka kwa wazazi wake. Na kitaka msingi huu ndipo wazazi wamelekezwa, *"Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee."* Mithali 22:6

*"21. Akawaambia wana wa Israeli akasema, Watoto wenu* ***watakapowauliza baba zao katika siku zijazo****, wakisema, Mawe haya maana yake ni nini? 22. Ndipo* ***mtakapowataarifu watoto wenu mkisema****...."* Yoshua 4:21-22

*"2. Sikilizeni haya,* ***enyi wazee****; Sikilizeni, enyi wenyeji wote wa nchi. Je! Mambo haya yamekuwako katika siku zenu, Au katika siku za baba zenu? 3.* ***Waarifuni watoto wenu*** *habari yake, watoto wenu wakawaambie* ***watoto wao****, Na watoto wao* ***wakakiambie kizazi kingine.****"* Yoeli 1:2-3

Kwa misingi hiyo ya kimaandiko utafahamu ya kwamba kinachotakiwa kutokea kweye umri wa utoto ni mafundisho na kuandaliwa kwa ajili ya maisha yajayo. Msingi wa haya mafundisho ni kwamba mtoto hafahamu yampasayo; haijui njia anayotakiwa kwenda; hajui uelekeo. Sasa jukumu la wazazi wake (mkazo uko kwa baba) ni kumwonyesha njia impasayo (siyo njia yoyote).

Vilevile, huu ndiyo umri ambayo mtoto anapaswa kurithishwa tunu za kimaisha. Hapa ninamaanisha

mabo ya kimsingi ambayo mara nyingi ahayafundishwi shuleni. Jukumu hili ni la wazazi na si mtu mwingine yeyote.

Kwenye awamu hii, mtoto hana maamuzi sana juu ya maisha yake. Mzazi ndiye anaamua mwenendo wa maisha ya mtoto. Sasa utaelewa maandiko yanamaanisha nini yasemapo "… na utukufu wa watoto ni baba zao."

Kwa ufupi: Ni kipindi cha utupu wa kiufahamu na jambo linapaswa kutokea ni kujazwa na maarifa na ufahamu.

### b) Awamu ya ujana

*"**Fahari ya vijana ni nguvu zao**, Na uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi."* Mithali 20:29

Hii ni awamu ambayo itazungumziwa kwa upana wake ndani ya kitabu hiki. Ni awamu ya nguvu!

Tazama maandiko yanasemaje hapa, "*tangu mwenye miaka ishirini umri wake , na zaidi, wote wawezao kutoka vitani katika Israeli…."* Hesabu 1:3. Ukikosma kitabu chote cha kutoka utagundua ya kwamba kwa kila kabila, kigezo cha umri wa miaka ishirini ndicho kilikuwa kipimo cha kuanzia kuingia jeshini kwa ajili ya kupigania nchi. Kwa lugha rahisi, ni sawa na kusema rika la jamii ya wamasai liitwalo "Morani".

Huu ni umri ambapo kijana anapswa aanze kujitegemea mwenyewe kiakili na kihisia. Umri wa kwenda kupigana vita si umri wa kusema, “mama yangu weeee!” siyo umri wa kuwa “mtoto wa mama”. Unatarajiwa siyo tu kujitegemea bali kuweza kusimama kwa ajili ya taifa lako. Na hapa ndipo dhana ya uzalendo inapozaliwa. Umri huu ndipo kijana analipenda taifa lake na anapaswa kufika mahali pa kuwa tayari kulifia. Anafuatilia maswala yenye mguso kwenye taifa lake.

Huu ndiyo umri ambao kijana anaweza kufuatilia maswala mbalimbali, kuyachambua na kuchukua maamuzi sahihi. Au unadhani kuwa mwanajeshi wa kwenda kupigania taifa vitani ni kujua kushika silaha na kufyatua risasi tu? La hasha!

Ni umri wa kuonyesha na kutumia nguvu zako. Huwezi kutumia nguvu hizo kabla (utotoni) kwa sababu hujazipata bado; na hauwezi kutumia baadaye (uzeeni) kwa sababu zitakuwa zimekwisha tayari.

Mpendwa wangu, wewe ni kijana? Hatuna umri mwingine wa kuleta mambo ya mlipuko… ni sasa au haitakuwa tena (It is now or never). Changa karata zako za awamu vyema! Roho anasema na kijana wa kitanzania.

c) Awamu ya uzee

*"Fahari ya vijana ni nguvu zao,* ***Na uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi.****"* Mithali 20:29

Halafu kuna hii awamu ya uzeeni. Binafsi, sijawahi kuwa mzee. Nimewahi kuwa mtoto; halafu nalikuwa kijana… na sasa ni kijana! Nitasema kama maandiko yasemavyo. Huu ni umri ambao utukufu wake uko kwenye mvi za kichwa. Kwa maana ya kwamba kwa kadiri umri unavyosogea, ndivyo nywele hubadilika rangi. Hivyo, mvi ni kuwakilisha uzoefu ambao mtu amejikusanyia kwenye safari ya maisha. Huu uzoefu unafaa sana kuwasaidia na kuwashauri wengine. Hata hivyo, mwenye mvi hana nguvu za kutekeleza alichokusanya uzoefu wake. *"… kabla hazijaja siku zilizo mbaya, Wala haijakaribia miaka utakaposema, Mimi sina furaha katika hiyo."* Mhubiri 12:1b. Ninajua unaamini kama mimi kuhusiana na uzee mwema, Hata hivyo, nguvu za ujana na uzee si sawa.

Kimuundo, umri wa uzee ndiyo jioni ya maisha ya mwanadamu. Hakuna tena awamu nyingine yoyote mbele yake ambayo anaiendea.

# Viwekezo ndani ya siku za Ujana:

a) Nguvu: *"Fahari ya vijana ni nguvu zao, Na uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi."* Mithali 20:29

Awamu ya ujana ni awamu ya nguvu. Na hapa ninakusudia kuzungumzia nguvu ya kuamuru matokeo. Ujana siyo sehemu ya "kusihi" matokeo. Kwenye awamu hii ni kipindi ambacho kijana anapaswa kutumia nguvu yake ya utashi na shauku kuu kulazimisha matokeo yawe halisi.

b) **Ujuzi**: Unawakumbuka vijana wane wa Kiebrania? Unawakumbuka vijana waitwao Meshaki, Shadraka, Abednego na Danieli? Biblia inasema hivi kuwahusu wao, *"Vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werevu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu…"* Danieli 1:4
Ndani ya kijana kuna uwezo wenye mfano wa mpira (rubber material) unaoweza kuvutika sana. Kwenye umri wa ujana unaweza kujifunza elimu, ujizi na maarifa yoyote. Kama kuna kitu nitakuambia uhakikishe unafanya, kusanya ujuzi. Jifunze mambo kwa wingi sana.

Lipa gharama za kifedha, muda na nafasi kujifunza. Huo uwezo umo ndani yako! Jifunze kwa njia ya elimu rasmi na kwa elimu isiyo rasmi.
Hitimisho kuhusu vijana hawa wa kiyahudi wakilinganishwa na wenye hekima wa Babeli likuwa hivi, *"Na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza mfalme, akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake."* Danieli 1:20

c) **Uwe wa kunyumbulika (flexibility):** Tumewatazama vijana wa Kiebrania na kuona jinsi walivyokuwa kiujuzi. Ninataka uone kutoka kwenye nchi yao ya Yuda kwenda Babeli lilikuwa badiliko kubwa sana. Waliingia kwenye utamaduni mpya, mifumo mipya, Imani nyingine, siasa tofauti… lakini walikuwa na uwezo wa kujifunza mambo mapya (siyo ya kuwatoa kwenye mikazo ya Imani) ili waweze kuishi kwenye eneo jipya. *"… tena alimwambia awafundishe elimu ya Wakaldayo, na lugha yao."* Danieli 1:4b Hivi unaelewa ilivyo kazi kujifunza lugha ngeni? Kwa kadiri umri unavyoenda, uwezo wa kujifunza lugha mpya unafifia… isipokuwa kama Roho Mtakatifu atavuvia kunena kwa lugha za wanadamu. Sasa,

hawa vijana sit u kwamba walifundisha lugha bali na elimu kwenye mfumo wa Wakaldayo. Kwa wale wanaofahamu kuhusu mifumo ya kielimu, utagunduanya kwamba ukienda ngazi ya juu kidogo ya elimu utafanyiwa "orientation course" ili uweze kuelewa nini kinaendelea kwenye ngazi husika. Sasa, ukienda kwenye nchi nyingine utagundua mfumo ni tofauti kabisa. Kuna watu huwachukua hata miezi sita kuelewa mfumo wa elimu. Hawa vijana walifundishwa elimu ya mfumo mwingine… ajabu na kweli wakafanya vyema kuwazidi hata wale waliolelewa kwenye mfumo huo!

Ninataka uone uwezo wao wa kunyumbulika (flexibility) ulivyokuwa ni mkubwa. Tahadhari yangu ni kwamba, tunaposema "flexibility" hatuna maana ya kuyapuuzia mambo ya msingi mathalani mambo ya kiimani. Misingi itunzwe! Hata vijana hawa walitunza misingi. Moja ya kitu kitakugharimu kama kijana ni kudhani unatunza misingi na kumbe umerukia awamu – uko uzeeni; au kudhani uko "flexible" na kumbe unafifisha mambo ya msingi. Mungu akupe hekima kuipita njia hiyo vyema.

d) Uthubutu: Moja ya kiwekezo kilichomo kwenye awamu ya ujana ni nguvu ya hali ya juu sana ya kuthubutu. Unamkumbuka Musa,

mkombozi wa taifa la Israeli? Alivyotoka kuwaona ndugu zake wakifanya kazi nzito za mawe na matofali? *"11. Hata siku zile, Musa alipokuwa mtu mzima, akatoka kuwaendea ndugu zake, akatazama mizigo yao. Akamwona Mmisri anampiga mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake. 12. Basi akatazama huko na huko, na alipoona ya kuwa hapana mtu, akampiga Mmisiri yule, akamficha ndani ya mchanga."* Kutoka 1:11-12

Ili uweze kuelewa vizuri andiko hilo, ni vyema ukalisoma pamoja na andiko hili, *"24.Akamwona mmoja akidhulumiwa, akamtetea, akamlipia kisasi yule aliyekuwa akionewa, akampiga huyo Mmisri. 25. Alidhani kwamba ndugu zake watafahamu ya kuwa Mungu anawapa wokovu kwa mkono wake, lakini hawakufahamu."* Matendo ya Mitume 7:24-25
Ukiisoma habari hii kwenye kitabu cha Kutoka na kuielewa kwa kitabu cha Matendo ya Mitume na Waebrani 11:25-27, utagundua yale matukio hayakuwa yanatokea tu. Kumbe Musa alikuwa na nia ndani ya moyo wake ya kuwakomboa ndugu zake, Waebrania. Na njia aliyoamua kuitumia ni kuua Mmisiri mmoja

mmoja mpaka ndugu zake wawe huru. Alikusudia kuwaletea ndugu zake ukombozi.

Huwa ninajiuliza ni ujasiri kiasi gani huo? Aliamua kuthubutu pakubwa na kuhatarisha maisha yake pakubwa sana.
Mungu alivyoona uthubutu huo akaupenda. Ndiyo akamtumia huyo huyo kuleta umbozi. Alimwita Midiani ili kurekebisha mitazamo siyo uthubutu!

Kijana, hakikisha umefika mahali hapo… hakikisha unaweza kuhatarisha mambo yako. Mimi ni na ushuhuda kwenye eneo hili. Si mara moja, nimehatarisha maisha na mambo yangu mengi kwa ajili ya injili…. Matokeo yake hayakanushiki! Ni vile unajihurumia sana ndiyo maana una mambo ya "kizee".

# Kuna mambo ni ya Ujana tu:

“Ni vema mwanadamu aichukue nira **wakati wa ujana wake.**” Maombolezo 3:27

Umewahi kufahamu kushus nira? Ni kifaa kinachotumika kuwavika wanyama shingoni kkisha hupelekwa ama kubeba mizigo au kufanya shughuli za kilomo. Sasa, Nabii Yeremia anaonyesha ya kwamba kuichukua nira swala la kujadili “ni vema” – inapaswa kuwa hivyo. Mjadala uko kwenye lini aichukue nira.

Kabla hatujaenda na swala la lini kwa kina kiasi, tujenge uelewa wa pamoja kuhusu nira.

- Majukumu na wajibu binafsi: Mnyama yeyote anapovikwa nira, havikwi kama mapambo. Hakuna mmiliki wa mnyama anayemvika nira kisha kuona amependeza kiasi gani. Hapana! Nira inaashilia muda wa kazi umewadia. Muda wa kuingia shambani au kubeba mizigo u karibu kuanza. Na hakuna mnyama ambaye huvikwa nira kwa niaba ya mwingine au kwa ajili ya mwingine. Kila mmoja ana sehemu yake inayotarajiwa katika swala la nira. Kwa uelewa huo, ndivyo yalivyo maisha; na ndivyo ulivyo ujana. Ndiyo kipindi cha kuchukua wajibu kamili. Hakuna mtu atachukua kwa ajili na/au

kwa niaba yangu. Usiwahi kujidanganya ya kwamba kuna mtu kutoka mahali fulani ataichukua nira kwa ajili yako. Usithubutu kuwaza ni baba, mama, jamaa au serikali. Hakikisha unaichukua nira yako mwenyewe!

- Nidhamu: Mnyama akifungwa nira, mara moja maisha yake yanapaswa kuchukua mkondo wa nidhamu. Mnyama hawezi kuwa kwenye safu ya kilimo au kubeba mizigo halafu akataka kwenda njia yake, kupumzika tu, au kufanya atakayo. Uhuru binafsi unaodoka baada ya kuvikwa nira. Ukisikia kuna ng'ombe ameonekana anazurura mahali fulani, hauhitaji nabii kukuambia ya kwamba hana nira! Ukiona kijana yuko kila mahali, anafanya kila jambo – "mwangalie shingoni", hana nira! Hakuna sehemu ya kujenga nidhamu kama sehemu hii iitwayo ujana.

- Kufikia mwisho: Kuvaa nira huambatana na lengo. Kama nilivyodokeza hapo awali ya kwamba nira siyo pambo la shingoni; siyo vazi tu. Nira huja baada ya lengo kujulikana. Inawezekana ni kulima kiasi fulani cha shamba; kubeba kiasi fulani cha mzigo na kwenda nao umbali fulani. Halafu baada ya lengo

kutambulika, nira haiondoki shingoni mpaka hapo lengo litakapokuwa limefikiwa. Kuna msemo wa kawaida nimewahi kuusikia *"Afe punda, zmigo ufike."* Huu uliundwa kukazia kwenye umuhimu wa lengo la mzigo kufika. Rafiki, kama ndani yako huoni umuhimu wa kufika mwisho, hutaivaa nira tangu awali. Ukweli ni kwamba hatujaja duniani kutembea tu… hatujaja kukutana na watu au kuzaliana. Kuna mwisho tumekusudiwa kuufikia. Kwenye umri huu wa ujana, pania ya kwamba utajua lengo, utavaa nira halafu utahakikisha mzigo unafika!

- Kuwa na matokeo: Kuvaa nira kunaashiria kusudio la kupata matokeo. Hapa ni tofauti na kufika mwisho/lengo. Kuna matokeo fulani yamekusudiwa – inawezekana na ndani ya kiwango fulani cha muda, kwa kipimo/kiasi fulani. Kuvaa nira ni ujumbe ya kwamba "nipo tayari kwa ajili ya matokeo."

Kwa taarifa yako, muda wa kuvaa nira ni SASA!

Hakikisha kwenye umri wa ujana umeanza kufahamu uelekeo wa maisha yako. Usijicheleweshe kwa kuvuta muda. Huna maisha mengine. Kama uelekeo wa maisha yako ni kwenye huduma ya madhabahuni,

wala *“usipake rangi”* wewe anza kuibeba nira yako asubuhi na mapema. Ruhusu maisha yako yaanze kuwa na *“sense of direction”* mapema iwezekanavyo.

## Hitimisho:

Bwana Uliyewaita, Watakatifu wako
Wawe mitume wachunga, walishe kundi lako
Wanyonge na wenye hofu, wakawa mashujaa
Na wapole wa kunena, wasiwe kunyamaa

Hata leo wawataka watakatifu wako
Nawe wauliza tena, ni nani alyeko
Atakaye nimtume afundishe vijana
Ni tayari BWANA wangu nitume mimi hapa

Nitume na mimi BWANA kama ulivyotumwa
Habari ya msamaha na dhambi kutubiwa
Niwahubiri wakosa na waliopotea
Wokovu u wake BWANA aliyewafilia
(Tenzi za Rohoni, #67)

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH *Dodoma*

# Abudu Nasi

**KILA JUMAPILI - saa 3.00 asbh -6.30 mch**

**KILA ALHAMISI - saa 11.00 jioni -12:15 jioni**



nvc_dodoma    +255 754 917 764

Mahali tulipo: **Swaswa - Njia Panda ya Waziri Mkuu**

*A Home of Impact*

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764